22:2-29:30 MAANDALIZI YA KUJENGA HEKALU

Daudi amtia moyo Sulemani (22:2-19) Makusudi ya Mungu yalikuwa kwamba Sulemani ajenge hekalu wala si Daudi. Ingawa Daudi alielewa sababu ya uamuzi huo naye aliukubali kwa unyenyekevu wake, lakini hata hivyo alifanya yote aliyoweza ili kumsaidia Sulemani katika kazi hiyo kubwa. Alikusanya vifaa vya ujenzi kwa wingi sana, akiwaweka wageni wote walioishi katika Israeli wafanye kazi ya kuandaa mawe kwa ajili ya jengo (2-5). Zaidi ya yote, alimwonya Sulemani atafute hekima kwa Mungu na kutii mapenzi yake, ili aweze kutawala Israeli kadiri ya sheria yake (6-13). Pia Daudi alimsaidia Sulemani kwa kumpatia mafundi wa kila fani wawe tayari kuanza kazi wakati wake (14-16)

Ushindi wa Daudi wa kila mahali ulikuwa umelipa taifa la Israeli nguvu sana, hata lisishambuliwe na adui ye yote kwa rhuda mrefu. Hali hiyo ilimpa Sulemani nafasi kutia mkazo wote katika miradi yake ya ujenzi bila ya kuzuiwa (17-19).

Mipango kwa ajili ya Walawi (23:1-26:32)

Baada ya kumweka Sulemani awe mrithi wa kiti cha enzi, Daudi alifanya mipango mingine kwa huduma ya hekaluni ya hapo baadaye. Kwanza, alifanya mpango wa kugawanya huduma mbalimbali kati ya Walawi. Sensa ya Walawi ilionyesha kwamba walikuwepo Walawi 38 000 waliofaa kwa huduma ya hekaluni. Kati ya hao 14 000 walikuwa maafisa wa kuandika habari, mahakimu, walinzi, waimbaji na wapigaji vyombo vya muziki. Walawi wengine 24 000 walipangwa ili wasaidie katika huduma ya kawaida ya hekaluni (23:1-6). Ni wazi kwamba walizidi kuwa wengi kwa kuhudumia hekaluni kwa wakati mmoja. Kwa hiyo Daudi aliwagawa katika vikundi kadiri ya nyumba zao, jumla yakawa makundi 24 (7-23).

Kila kundi lingepaswa kuhudumia hekaluni kwa majuma mawili kila mwaka (Hivyo huduma ya majuma 48 ilipatikana. Majuma manne ya mwaka yaliyobaki yangechukuliwa na sikukuu za Pasaka, Pentekoste na Vibanda. Katika sikukuu hizo wanaume wote wa Israeli walipaswa kukutana Yerusalemu kwa ibada rasmi, kwa hiyo hata Walawi wote walitakiwa kazini; taz.Kut 23:14-17.) Kazi ya Walawi ilikuwa kuwasaidia makuhani, kutunza usafi wa hekalu, kuimba katika ibada mbalimbali na kushughulika katika mambo ya sadaka na sherehe zote (24-32).

Makuhani pia waligawanywa katika makundi 24, kila kundi likitumia majuma mawili kila mwaka, kama ilivyoonyeshwa hapo juu. Huduma hiyo walipokezana watu wa tawi la Eleazari na tawi la Ithamari la ukoo wa Haruni. Muda wa huduma ya kila kuhani ulichaguliwa kwa njia ya kura (24:1-6). Kisha makundi 24 ya makuhani yaliorodheshwa (7-19). Orodha nyingine ya baadhi ya Walawi ikafuata (20-31).

Katika waimbaji wa hekaluni 4000 (taz.23:5), 288 walikuwa wataalamu wa kupiga muziki waliokuwa wamefundishwa sana, pamoja na viongozi wao 24 (25:1-7). Wataalamu wale wa muziki 288 pia waligawanywa katika vikundi 24 vilivyopaswa kuhudumia kwa zamu. Kazi yao ilikuwa kufundisha na kuongoza waimbaji wa sehemu hizo walizopangiwa (8-31).

Pia walikuwepo mabawabu au walinzi wa hekaluni 4000 (taz.23:5). Inavyoonekana hata wao waligawanywa katika vikundi 24 vilivyofanya kazi yao kwa zamu. Zilikuwepo sehemu 24 zilizotaka kulindwa (26:1-19). Mali ambayo Daudi na wengine walipata kwa njia ya mateka yao, ilitunzwa kwa uangalifu sana na kundi la maakida (au wahasibu) ambao majina yao yaliorodheshwa (20-28). Mahakimu 6000 (taz.23:4) labda walipangwa, ili wafanye kazi zao kwa zamu. Baadhi yao walishughulika na utawala wa serikali kuu, ambapo wengine walifanya kazi magharibi na wengine mashariki ya Yordani tu (29-32).

Viongozi wa kijeshi na wa kiraia (27:1-34) Kinyume cha maelezo ya kinaganaga ambayo mwandishi alitoa kuhusu orodha za Walawi, alijumlisha viongozi wa kijeshi na wa kiraia wa Daudi kwa kifupi sana. Kila mwezi wanaume 24.000 walipaswa kuhudumia jeshini kwa muda wa mwezi mmoja. Majemadari 12 walioongoza jeshi pia walishika zamu katika huduma yao. Wote walikuwa watu wa kundi la Daudi la 'mashujaa wake' (27:1-15; taz.l 1:10-47). Orodha nyingine tatu zilitaja viongozi wa makabila mbalimbali (16-24), maafisa walioangalia mashamba ya mfalme (25-31) na washauri waliokuwa karibu sana na mfalme (32-34).

Daudi amweka Sulemani mbele ya watu (28:1-29:30)

Sulemani alikuwa amepakwa mafuta haraka kuwa mfalme ilipojulikana kwamba Adonia alitaka kujipatia kiti cha enzi kwa nguvu (taz. maelezo ya lFal 1:5-53). Kupakwa mafuta kwa Sulemani bila sherehe maalumu kulifuatwa na sherehe rasmi ya hadharani ya kupakwa mafuta tena, wakati huo

mambo yote ya kidini pia yakitimizwa (taz.29:22). Tukio hilo linaelezwa hapa. Daudi alimweka Sulemani mbele ya watu akiwa ndiye aliyechaguliwa na Mungu awe mfalme badala yake na kulijenga hekalu (28:1-10). Kisha Daudi alimpa Sulemani ramani yake ya kujenga hekalu na mipango yake kuhusu ibada zote za hekaluni. Alimtia moyo Sulemani ili aendelee na kazi yake mpaka kumaliza hekalu na kulitumia kadiri ya mipango aliyofanya (11-21).

Licha ya fedha na vifaa ambavyo alikuwa amekwisha toa kwa ujenzi huo (22:14), Daudi pia alitoa sadaka kubwa sana kutoka katika fungu lake binafsi. Kielelezo chake kiliwahamasisha watu hata wao watoe sadaka nyingi na kubwa (29:1-9). Mwitikio wa furaha kutoka kwa watu ulimsababisha Daudi kutoa sifa kubwa ya ghafla kwa Mungu. Alikubali kwa furaha kwamba vitu vyote ambavyo wanadamu wanaweza kuwa navyo vinatoka kwa Mungu. Kwa hiyo Waisraeli walipotoa sadaka kwake walimrudishia vitu vile tu ambavyo Yeye aliwapa katika kwanza. Walifanya hivyo kwa furaha na kwa hiari yao, na Daudi akaomba kwamba Mungu awasaidie waendelee kujitoa kwake namna hiyo siku zote (29:10-19).

Siku ya pili yake watu walishirikiana naye sherehe kubwa sana, wakaapa uaminifu wao kwa Sulemani akiwa mfalme wao mpya (20-25). Kabla ya kuendelea na habari za Sulemani, mwandishi alijumlisha kwa kifupi tena utawala wa Daudi (26-30).